JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'
Simu: 0222131070
Fax: 026 2136924

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi
Mtaa wa Nzuguni A
P.O. Box 2851
**41220- DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

### Kukanusha Upotoshaji na Kueleza Msimamo wa Msajili wa Vyama vya Siasa Kuhusu Malalamiko ya Bwana Lembrus Mchome

Zimekuwepo taarifa za kupotosha kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kuhusu maamuzi na maelekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa yaliyohusu uhalali wa kikao cha Baraza Kuu la Taifa la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilichofanyika tarehe 22 Januari, 2025.

Kwa nyakati tofauti baadhi ya watu wamesikika wakisema kuwa, Bwana Lembrus Mchome alisaidiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuandaa na kuwasilisha malalamiko yake dhidi ya chama chake cha CHADEMA. Madai hayo hayana ukweli wowote.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inapenda kuwafahamisha wananchi kuwa, suala la kuhoji uhalali wa kikao cha Baraza Kuu la Taifa la CHADEMA cha tarehe 22 Januari, 2025 na maamuzi ambayo kikao hicho kilifanya, linatokana na malalamiko ya mwanachama wa CHADEMA Bwana Lembrus Mchome ambaye aliwasilisha kwa barua ya tarehe 15 Machi, 2025. Kwenye barua yake alikuwa na hoja tatu ambazo ni:-

(i) Kutotimia kwa akidi ya kikao.
(ii) Uwepo wa watu ambao siyo wajumbe wa kikao kwenye ukumbi wakati wa kupiga kura.
(iii) Watu ambao siyo wajumbe kupiga kura.

Siyo mara ya kwanza Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kupokea malalamiko kama hayo. Pamoja na Lembrus Mchome, wapo wanachama wengine wa vyama

vya siasa ambao wameshawahi kuwasilisha malalamiko kwa Msajili wa Vyama vya Siasa wakilalamikia vyama vyao kuhusu ukiukaji wa Katiba na Kanuni za chama. Hivyo, alichofanya Bwana Lembrus Mchome siyo kitu kipya au cha ajabu.

**Madai ya Chadema Dhidi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa**

1. CHADEMA inadai kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilikuwepo katika kikao hicho. Ukweli ni kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilikuwepo katika Mkutano Mkuu wa CHADEMA wa tarehe 21 Januari, 2025, lakini haikualikwa na haikuwepo katika kikao cha Baraza Kuu la Taifa la CHADEMA cha tarehe 22 Januari, 2025 kilicholalamikiwa na Bwana Mchome.

2. Hoja nyingine ya CHADEMA ni kuwa, Bwana Mchome aliwasilisha rufaa na siyo malalamiko. Baada ya kuchambua barua zake na maelezo ya CHADEMA, Msajili wa Vyama vya Siasa alijiridhisha kuwa, alichowasilisha Bwana Mchome ni malalamiko na siyo rufaa. Hivyo, madai hayo hayana mantiki.

3. Aidha, hoja ya CHADEMA kwamba, Bwana Mchome alipaswa kuwasilisha malalamiko yake ndani ya chama kabla ya kuyawasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Hoja hii pia haina mantiki kwa sababu hakuna sheria inayoelekeza hivyo. Maamuzi ya Mahakama ambayo CHADEMA wameyaeleza katika barua yao kuhusu suala hili, yanahusu mwenendo wa Mahakama na siyo masuala mengine nje ya hapo.

4. Vilevile CHADEMA wanadai kuwa, Msajili wa Vyama vya Siasa hana mamlaka ya kufanyia kazi malalamiko ya mwanachama wa chama cha siasa yanayohusu ukiukwaji wa Katiba na Kanuni za chama na kutoa uamuzi na maelekezo. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilitoa ufafanuzi wa kina kuhusu suala hili katika barua yake kwa CHADEMA ya tarehe 08 Aprili, 2025 yenye kumbukumbu namba HA. 322/362/16/130. Katika barua hiyo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilinukuu vifungu vya Sheria vinavyompa Msajili mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Katiba na Kanuni za vyama vya siasa na kuchukua hatua endapo kutakuwa na ukiukwaji.

5. Kuhusu madai kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilifanyia kazi malalamiko ya Mchome kwa kusikiliza upande mmoja na kutoa uamuzi wake. Ukweli ni kwamba, baada ya kupokea malalamiko hayo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliuandikia barua uongozi wa CHADEMA kuwataka

wawasilishe maelezo na ushahidi wao dhidi ya hoja zilizowasilishwa na Bwana Mchome, lakini walikataa kufanya hivyo wakieleza kuwa, Msajili wa Vyama vya Siasa hana mamlaka ya kusikiliza malalamiko hayo.

Vitendo vya kukaidi maagizo ya Msajili wa Vyama vya Siasa viliendelea kujitokeza ambapo tarehe 25 Mei, 2025, Makamu Mwenyekiti Bara wa CHADEMA wakati akisoma maazimio ya kikao cha Kamati Kuu kilichofanyika tarehe 23 na 24 Mei, 2025 Dar-es salaam alieleza kwamba, kikao hicho kimeazimia kuwa, maamuzi na maelekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu malalamiko ya Bwana Mchome ni batili na hawatoyafanyia kazi. Napenda kuwafahamisha Watanzania kuwa, Msajili wa Vyama vya Siasa amesikitishwa na msimamo huo wa CHADEMA, kwa sababu wanapaswa kufanya uamuzi wa busara wa kuitisha kikao halali cha Baraza Kuu la Taifa la chama chao na kujaza nafasi zilizowazi, badala ya kubishana na sheria, kwani sheria ni msumeno.

Kwa mnasaba huo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inapenda kuwafahamisha wananchi, wadau, mamlaka na taasisi zote za Serikali na binafsi kuwa,

a) Wanachama walioorodheshwa hapo chini siyo viongozi wa CHADEMA:-

   i. Bwana John John Mnyika;
   ii. Bwana Amani Golugwa;
   iii. Bwana Ali Ibrahimu Juma;
   iv. Bwana Godbless Jonathan Lema;
   v. Dkt. Rugemeleza Albert Nshala;
   vi. Bi. Rose Mayemba;
   vii. Bi. Salima M. Kasanzu;
   viii. Bwana Hafidhi Ali Saleh;
   ix. Viongozi na watendaji wote walioteuliwa na viongozi waliopatikana katika kikao cha Baraza Kuu cha tarehe 22 Januari, 2025; na
   x. Viongozi na watendaji wote walioteuliwa kwa mamlaka za chama kushauriana na viongozi waliopatikana katika kikao cha Baraza Kuu cha tarehe 22 Januari, 2025.

b) Aidha, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inawasihi wananchi, wadau, mamlaka na taasisi zote za Serikali na binafsi, kutowapa ushirikiano na huduma wanachama walioorodheshwa hapo juu, endapo watahitaji kuzipata kama viongozi wa CHADEMA. Kwa mujibu wa kifungu cha 4(5)(a)(b), 8B, 10(f) vya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 na Kanuni ya 31 ya Kanuni

za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka, 2019 (The Political Parties (Registration and Monitoring) Regulations, 2019 GN. 953) viongozi halali wa vyama vya siasa ni wale wanaotambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa;

c) Kutokana na ombwe la uongozi lililobainishwa hapo juu, Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mamlaka aliyonayo chini ya kifungu cha 18(6) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, ameamua kusitisha kuwapa ruzuku CHADEMA hadi watakapotekeleza maelekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa sababu chama hicho hakina viongozi wanaoweza kusimamia mapato, matumizi na marejesho ya fedha hizo za umma;

d) Endapo CHADEMA wataendelea kukaidi kutekeleza maamuzi na maelekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza kuchukua hatua zifuatazo:

    (i) Kuzitaka mamlaka husika zichukue hatua za kisheria za kijinai kwa mujibu wa kifungu cha 8B cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kwa wahusika wanaojinasibu kuwa ni viongozi; na

    (ii) Kuwasimamisha wanaojifanya kuwa ni viongozi kufanya shughuli za kisiasa kwa mujibu wa kifungu cha 21E cha Sheria ya Vyama vya Siasa.

Vilevile Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inapenda kuwakumbusha wanachama na viongozi wa CHADEMA kuwa, kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya Vyama vya Siasa anayo mamlaka ya kusimamisha usajili wa chama hicho, endapo kitaendelea kuwatambua wanachama waliotajwa hapo juu kuwa ni viongozi wa chama hicho.

Mwisho, Ofisi inaviasa Vyama vya Siasa kuheshimu na kutekeleza sheria ya vyama vya siasa na sheria nyingine za nchi, ili kuepuka misuguano na mivutano isiyokuwa ya lazima.

Abuu M. Kimario

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO NA ELIMU YA URAIA**

27 Mei 2025